

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

Simu: 0262126826  
Nukushi: 026 2126834  
Barua pepe: km@michezo.go.tz  
Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali,  
Mtumba, Dodoma  
2 Mtaa wa Habari,  
S. L. P. 25,  
40481 DODOMA.

**TAARIFA KWA UMMA**

**UFAFANUZI KUHUSU UWANJA WA MKAPA**

**Februari 5, 2023 – Dodoma**

Wizara inapenda kutoa ufafanuzi kuhusu picha na taarifa zinazosambaa katika Vyombo vya Habari na Mitandao ya Kijamii yenye kichwa cha habari 'Uwanja wa Mkapa Unaanza Kutia Aibu'.

Ufafanuzi ni kuwa picha zinazotumika pamoja na ujumbe huo ni picha ambazo zilichukuliwa siku za nyuma (mara baada ya tukio la Mkesho lililofanyika tarehe 16/12/20 katika uwanja huo). Kufuatia hali hiyo iliyojitokeza wakati huo, Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ilichukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kuwa hali hiyo haijitokezi tena kama ifuatavyo:

1. Wizara ilifanya mabadiliko ya Menejimenti ya Uendeshaji wa Uwanja huo.
2. Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Ligi ambayo ndiyo mdau mkubwa imeandaa muongozo wa matumizi wenye lengo la kudhibiti masuala ya usafi.
3. Wizara imeunda kikosi kazi kidogo cha usafi na mazingira ambacho kinafanya ukaguzi wake kabla na baada ya uwanja kutumika ili kuimarisha usafi, na;
4. Wizara ilimuelekeza mzabuni wa uwanja huo kuboresha huduma ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya vibaru wa usafi wakati wa matukio.

Wizara inatoa rai kwa wadau wa michezo na umma wote wa wataanzania kushirikiana katika kuvitunza viwanja vyote kwa kuzingatia usafi wakati wa matumizi yake na kujiepusha na aina yoyote ya uharibifu.

Imetolewa na:

John Mapepele

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**